المجلس الأعلى للشئون الإسلامية بتنزانيا
BARAZA KUU LA WAISLAM TANZANIA ( BAKWATA )
THE NATIONAL MUSLIM COUNCIL OF TANZANIA

# KANUNI
# ZA
# UCHAGUZI - BAKWATA

**S.L.P 21422 DAR ES SALAAM**

**TOLEO LA MWAKA 2024**

## YALIYOMO


UTANGULIZI ........................................................ 1

TANBIHI ........................................................ 2

UONGOZI ........................................................ 3

**SURA YA KWANZA: KANUNI ZA JUMLA** ........................................................ 4

1: NAFASI ZA UONGOZI ........................................................ 4

2: VIKAO VYA KUCHUJA WAOMBAJI WA NAFASI ZA UONGOZI ........................................................ 5

3: VIKAO VYA UCHAGUZI ........................................................ 7

4: UTARATIBU WA KUPIGA KURA ........................................................ 9

5: UTARATIBU WA KUHESABU KURA ........................................................ 10

6: KUTANGAZA MATOKEO ........................................................ 11

7: NAFASI ZA UONGOZI WA KUTEULIWA ........................................................ 12

8: MALALAMIKO YA UCHAGUZI ........................................................ 13

9: MIIKO KATIKA SHUGHULI ZA UTEUZI NA UCHAGUZI ........................................................ 18

**SURA YA PILI: UCHAGUZI WA VIONGOZI WA NGAZI YA MSIKITI** ........................................................ 21

10: MSIKITI ........................................................ 21

11: UTARATIBU WA KUOMBA UONGOZI NGAZI YA MSIKITI ........................................................ 21

12: UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA MSIKITI ........................................................ 22

**SURA YA TATU: UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA KATA** ........................................................ 23

13: UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI YA UONGOZI WA KATA ........................................................ 23

14: UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA KATA ........................................................ 24

**SURA YA NNE: UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA WILAYA** ........................................................ 26

15: UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI YA UONGOZI NGAZI YA WILAYA ........................................................ 26

16: UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA WILAYA ........................................................ 27

**SURA YA TANO: UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA MKOA** ........................................................ 29

17: UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI ZA UONGOZI NGAZI YA MKOA ........................................................ 29

18: UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA MKOA ........................................................ 30

**SURA YA SITA: MKUTNO MKUU WA TAIFA NA MENGINEYO** .......................... 32

19: MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA TAIFA .................................................... 32

20: UCHAGUZI WA KUJAZA NAFASI ZILIZOACHWA WAZI ................................... 32

## UTANGULIZI

Sisi Waislamu wa Tanzania kwa kuwa tunaamini kama Waislamu wengine wote Ulimwenguni, kwamba hakuna apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake, na kwamba Muhammad (swalla llahu alaihi wasalaam) ni Mtume wake wa mwisho na hapana tena mtume mwingine baada yake. Kwamba Qur'an na Sunna ndiyo vitu viwili vikubwa ambavyo Mtume Muhammad (swalla llahu alsaihi wasalaam) ameviacha kwa Umma wake, na kwamba ili tuongoke ni lazima tuvisome, tuvizingatie na tuvifuate kama inavyopaswa kufuatwa.

Tangu kuanzishwa kwa BAKWATA mwaka wa 1968, misingi na utaratibu wa kuwapata viongozi wetu kuanzia ngazi ya Msikiti hadi Taifa umekuwa madhubuti na wenye kufuata haki. Viongozi wote wa kuchaguliwa na kuteuliwa wamekuwa wakifanya kazi kwa kujitolea kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Kufanya kazi kwa kujituma na kujitolea ndio muhimili wa dhati wa kuendeleza na kukuza maadili ya dini yetu tukufu ya Kiislamu. BAKWATA itahakikisha kuwa utaratibu na msimamo huu wa kujituma na kujitolea unaendelezwa kwa maslahi ya taasisi yetu na Uislamu kwa ujumla.

**TANBIHI**

i. Katika kuimarisha kazi yake ya kuongoza na kuwahudumia Waislamu wa Tanzania, BAKWATA haina budi kuhakikisha kuwa viongozi wake wote, wakuchaguliwa na wakuteuliwa ni Waislamu wanaofuata mafundisho ya Qur'an tukufu na mwenendo wa Bwana Mtume Muhammad (swalla llahu alaihi wasalaam)

ii. Kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA, Uchaguzi Mkuu hufanyika kila baada ya kipindi cha miaka mitano (5).

iii. Ili tuweze kupata ufanisi zaidi katika chaguzi zetu sharti tufanye juhudi ya kuepuka kasoro zote zinazogusa maadili ya Uislamu na zile za utendaji ambazo zinawezesha watu wasiostahili kuchaguliwa na waweze kuingia kwenye uongozi ama kwa rushwa au kwa hila. Kwa sababu hiyo lazima maadili na murua wa Kiislamu uzingatiwe kwa ukamilifu na vikao vyote vinavyochuja na kuteua wagombea.

iv. Aidha pamoja na kuwapo kwa kanuni hizi, Katibu Mkuu wa BAKWATA anaweza kutoa miongozo ya ziada kuhusu masuala yanayopaswa kuzingatiwa katika chaguzi za BAKWATA.

v. Wajibu wa BAKWATA wakati wote ni kujenga, kusimamia na kudumisha uongozi bora nchini. Uongozi bora ni moja ya misingi wa kudumisha haki na kuleta maendeleo ndani ya BAKWATA na Waislamu wote nchini.

## UONGOZI

Uongozi mzuri na bora katika taasisi yetu unaegemezwa katika mafundisho ya Qur'an na Sunna pamoja na kufuata masharti yafuatayo:

(a) Kiongozi wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) ni lazima afuate muongozo wa Qur'an na mafundisho ya Bwana Mtume Muhammad (swala llahu alaihi wasalaam).

(b) Awe ni mwenye kuikubali na kuifuata katiba ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA)

(c) Awe ni mwenye maadili na tarbiya ya Kiislamu kwa mujibu wa mafundisho ya Bwana Mtume Muhammad (swalla llahu alaihi wasalaam)

(d) Awe na uwezo wa kazi anayotarajia kufanya katika ngazi anayoomba kuchaguliwa.

(e) Awe na uwezo wa kusimamia, kufuatilia na kutatua matatizo ya waliomwamini na kumchagua.

(f) Kila kiongozi ni lazima achaguliwe na waumini kwa hiari na ridhaa yao na kwa njia ya haki kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.

(g) Muda wa Uongozi katika nafasi zote za kugombea ni miaka mitano.

## SURA YA KWANZA
## KANUNI ZA JUMLA

### 1. NAFASI ZA UONGOZI

**a.** Mheshimiwa Mufti, ambae ni miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Ulamaa anapatikana kutokana na mapendekezo ya Tume ya Dini na kuthibitishwa katika Mkutano Mkuu kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA.

**b.** Tume ya Dini inajumuisha Masheikh wote wa Mikoa na wilaya za Tanzania Bara ambao kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA 1999 toleo la 2018 wanateuliwa na Baraza la Ulamaa.

**c.** Wajumbe wa Baraza la Ulamaa na Wadhamini wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) ambao wanapatikana kutokana na uteuzi wa Mheshimiwa Mufti na kuthibitishwa katika mkutano mkuu kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA.

**d.** Viongozi wafuatao wanachaguliwa kwa kufuata taratibu zifuatazo:-

i. Maimamu wa Misikiti wanateuliwa na Baraza la Masheikh la Wilaya.
ii. Masheikh wa Kata wanaoteuliwa na Baraza la Masheikh la Mkoa.
iii. Masheikh wa Wilaya na Mkoa wanaoteuliwa na Baraza la Ulamaa.

**e.** Kila Muislamu anayeomba nafasi yoyote ya Uongozi katika ngazi nyengine yoyote tofauti na walioanishwa na kutajwa katika kanuni hizi watatakiwa kwanza kujaza fomu ya

kuomba nafasi ya uongozi anayotaka kutoka katika ofisi za ngazi husika ikiwemo ya Msikiti, Kata, Wilaya na Mkoa. Baada ya kujaza itabidi airudishe katika ofisi alipoichukua kwa kufuata na kuzingatia muda uliowekwa. Fomu zote za kuomba nafasi za uongozi zinatolewa kwa kuchangia gharama.

**f.** Kutakuwa na fomu za uongozi wa aina zifuatazo:

i. Fomu za kuomba uongozi wa BAKWATA katika ngazi ya Msikiti
ii. Fomu za kuomba uongozi wa BAKWATA katika ngazi ya Kata
iii. Fomu za kuomba uongozi wa BAKWATA katika ngazi ya Wilaya.
iv. Fomu za kuomba uongozi wa BAKWATA katika ngazi ya Mkoa

## 2. VIKAO VYA KUCHUJA WAOMBAJI WA NAFASI ZA UONGOZI

**a.** Waombaji wote wa nafasi za uongozi watachujwa na vikao vinavyohusika katika ngazi hiyo au vikao vya juu kama inavyofafanua katiba. Wajumbe katika vikao vya uchujaji watajadiliana kuhusu Elimu, Ujuzi, Uzoefu, maarifa na maadili kama ilivyoainishwa katika ibara ya 80, Sehemu ya Nne ya katiba ya BAKWATA ya mwaka 1999, toleo la 2018. Baada ya kikao kujiridhisha kitapitisha jina au majina na kuyawasilisha kwa mamlaka husika kwa ajili ya kutoa idhini ya uchaguzi.

**b.** Vikao vya kuwachuja waombaji wa nafasi mbalimbali za uongozi utafanyika kwa kufuata ratiba iliyotolewa kwaajili hiyo. Kikao cha kuwachuja waombaji wa nafasi mbalimbali za uongozi kitasimamiwa na Wajumbe wa Baraza la Masheikh wa ngazi ya juu yake kwa muongozo wa katiba.

**c.** Baada ya muombaji kujadiliwa, maoni na mapendekezo ya kikao cha juu yaandikwe kwenye kumbukumbu za kikao na kwenye fomu yake aliyoijaza na atapewa alama inayolingana na maelezo aliyoyatoa. Alama zitakazotumika ni A, B, C, D na E.

**d.** Alama **"A"** itatolewa kwa muombaji anayetimiza maadili, masharti na sifa zote za Uongozi kama ilivyoainishwa katika ibara ya 80 ya sehemu ya Nne ya katiba ya BAKWATA.

i. Awe ni mwenye kujituma na kujitolea ili kufanikisha Majukumu yake.
ii. Awe ni mwenye nidhamu na kufuata utaratibu wa uongozi ulioanishwa katika katiba.
iii. Awe muaminifu na muadilifu katika tabia na mwenendo na anayechunga nidhamu na maadili ya Kiislamu.
iv. Awe tayari kushirikiana na Viongozi wenzake katika Kuendeleza na kufanikisha malengo ya taasisi na Uislamu kwa ujumla.
v. Awe na uwezo wa utendaji katika nafasi aliyoiomba kutokana na uzoefu.
vi. Awe anaonyesha kwa vitendo na nadharia uwezo wake katika kubuni, kuandaa watu, kuweka malengo, kusimamia utekelezaji wake na kupima matokeo ya utekelezaji wake.
vii. Awe tayari wakati wote kujikosoa, kukosolewa, na kuelekezwa kama mbinu ya kujiimarisha katika utendaji wake.

**e.** Alama **"B"** itatolewa kwa muombaji anayetimiza sifa na masharti yote ya uongozi lakini anapungukiwa na moja ya sifa za nyongeza (vi) na (vii)

**f.** Alama **"C"** itatolewa kwa muombaji anayetimiza sifa na masharti lakini msimamo wake na uwezo wake ni wa wastani.

**g.** Alama **“D”** itatolewa kwa muombaji ambaye hana dosari lakini uwezo wake ni mdogo wa kuweza kutekeleza na kumudu majukumu.

**h.** Alama **“E”** Itatolewa kwa muombaji ambaye ameonekana ana dosari za kimaadili na kiutendaji.

**i.** Ili kuziba mwanya wa kuweza kughushi maelezo na alama za muombaji yeyote nje ya kikao, maelezo na alama itakazotolewa kwa kila muombaji zitathibitishwa kwa kusainiwa na mwenyekiti na katibu wa kikao kilichohusika kabla ya kufunga mkutano wake.

**j.** Vikao vyote vya uchujaji na uteuzi wa wagombea wa ngazi zote ni lazima kuzingatia kukamilisha akidi ambayo ni nusu ya wajumbe wakati wa kutimiza majukumu yao.

**k.** Majina ya wagombea yaliyopitishwa baada ya uchujaji katika ngazi ya mkoa yatapelekwa katika ngazi ya Taifa ili kuhakiki na kukamilisha zoezi la uteuzi na uchujaji kabla ya kurudisha majina ya wagombea walioteuliwa kwa ajili ya uchaguzi.

**l.** Hairuhusiwi muombaji wa nafasi yoyote ya uongozi kuondoa jina lake baada ya kuteuliwa kugombea bila ya idhini ya kikao kinachofanya uteuzi wa mwisho.

## 3. VIKAO VYA UCHAGUZI

**a.** Vikao vya uchaguzi vitafanyika kwa kufuata ratiba itakayotolewa kwa ajili ya uchaguzi unaohusika. Ni marufuku kufanya kampeni ya aina yoyote.

**b.** Kila kikao cha uchaguzi kitasimamiwa na Msimamizi wa uchaguzi wa Msitiki, Kata, Wilaya au Mkoa kwa niaba ya Katibu Mkuu ambaye ndie msimamizi mkuu wa uchaguzi au mjumbe yeyote atakaeteuliwa na Katibu mkuu.

**c.** Mjumbe ambaye ni mgombea wa nafasi yoyote ya uongozi hataruhusiwa kuwa Mwenyekiti wa muda au kiongozi wa aina yoyote katika mkutano huo wa uchaguzi. hatakuwa na haki ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda katika mkutano huo.

**d.** Kazi ya wasimamizi hao itakuwa ni kuhakikisha kuwa haki inatendeka na kwamba maagizo ya Katiba ya BAKWATA pamoja na Kanuni hizi yanafuatwa kwa ukamilifu.

**e.** Wasimamizi wa uchaguzi pia watakuwa na uwezo wa kutoa uamuzi wa pamoja juu ya jambo lolote linalohusu utaratibu litakalotokea wakati wa Mkutano wa uchaguzi endapo jambo hilo halijafafanuliwa katika Kanuni hizi.

**f.** Wagombea wote walioteuliwa kugombea watapewa nafasi ya kujieleza mbele ya mkutano wa uchaguzi unaohusika.

**g.** Katika uchaguzi ambapo wanaohitajika kuchaguliwa ni zaidi ya mjumbe mmoja, kama vile wajumbe wa halmashauri za wilaya na mkoa, kila mpiga kura atapiga kura katika karatasi moja kwa idadi maalum inayotakiwa. Mpiga kura atakaepiga kura zaidi au pungufu ya kura zinazotakiwa, kura yake itakuwa imeharibika.

**h.** Katika uchaguzi wa kujaza nafasi nyingi kwa pamoja, endapo idadi ya wagombea walioteuliwa kwa ajili ya

uchaguzi wa nafasi hizo ni wachache kuliko nafasi zilizopo, au kama haizidi idadi ya nafasi hizo, wajumbe watapiga kura ya “ndiyo” au “hapana’ kwa kila mgombea.

**i.** Mwenye haki ya kupiga kura ni yule ambae ni mjumbe halali kikatiba wa Mkutano wa uchaguzi unaohusika.

**j.** Ili kuhakikisha kwamba watu wasiokuwa na haki ya kupiga kura hawapigi kura, Mikutano ya uchaguzi itahudhuriwa tu na wajumbe wa mkutano huo kwa mujibu wa Katiba ya BAKWATA, pamoja na maafisa wanaotakiwa kuhudumia mkutano huo na wasaidizi wao. Wajumbe wa kukaribishwa hawataruhusiwa kupiga kura. Endapo itakuwa lazima mikutano ya uchaguzi kuwa na wakaribishwa itabidi sehemu yao ya kukaa itengwe ili wasichanganyike na wajumbe wa mikutano. Wasimamizi na wengine wote wasio wajumbe hawatapiga kura. Karatasi za kupiga kura zisigawiwe mpaka wagombea wote wamemaliza kujieleza.

## 4. UTARATIBU WA KUPIGA KURA

**a.** Uchaguzi wote wa BAKWATA utafanyika kwa kura za siri kuanzia ngazi ya msikiti hadi Taifa kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa mapema kwa ajili hiyo. Kiwango cha mahudhurio ya wajumbe katika mikutano ya BAKWATA ya uchaguzi (akidi ya wajumbe) ni nusu ya wajumbe walio na haki ya kupiga kura katika Mkutano unaohusika kwa mujibu wa Katiba ya BAKWATA.

**b.** Katika uchaguzi wa BAKWATA wa ngazi zote, utaratibu wa kupiga kura utakuwa kwa kila mjumbe halali kupiga kura kwa uhuru. Kila mjumbe mwenye haki ya kupiga kura

katika uchaguzi huo, na kwa kufuata mpangilio uliowekwa, ataondoka mahali alipoketi na kwenda mahali maalum palipotengwa kwa ajili ya zoezi la upigaji kura. Mjumbe huyo atakabidhiwa karatasi moja ya kupigia kura, atapiga kura yake kwa siri, na kisha ataitumbukiza karatasi hiyo kwenye sanduku la kura litakalokuwa limewekwa mahali pa wazi.

**c.** Mikutano yote ya uchaguzi itaanza mapema iwezekanavyo kabla na siyo baada ya saa Nne asubuhi. Kwa hivyo maandalizi yafanywe kwa makini ili kuhakikisha kwamba wajumbe wahusika wanakuwa tayari katika viti vyao kabla ya saa iliyopangwa. Hatua hii ni kuepukana na tabia ya kufanya Mikutano ya uchaguzi usiku kwa sababu tu ya kuchelewa kuanza.

## 5. UTARATIBU WA KUHESABU KURA

Kazi ya kuhesabu kura itasimamiwa na kamati itakayokuwa imeteuliwa mapema chini ya usimamizi wa msimamizi wa uchaguzi.

**a.** Katika uchaguzi wa kujaza nafasi moja, ambapo wagombea hawawezi kuzidi watatu, kila mgombea anaweza kuteua mwakilishi wake mmoja kutoka miongoni mwa wajumbe wa mkutano unaohusika, atakaehudhuria kama mwakilishi wake katika zoezi la kuhesabu kura zinazomhusu. Hata hivyo, mgombea mwenyewe anaweza, akipenda kuhudhuria yeye mwenyewe katika zoezi la kuhesabu kura zinazomhusu.

**b.** Katika uchaguzi wa kujaza nafasi za makundi, hususani ya wanawake na vijana ambapo wagombea kwa kawaida huwa ni wengi kiasi kwamba haiwezekani kwa kila mgombea kupewa fursa ya kuteua mwakilishi wake, itabidi wagombea

wa makundi hayo wakubali kwamba kamati iliyoteuliwa kusimamia kazi ya kuhesabu kura ndiyo itakuwa mashahidi wao katika zoezi hilo au wapendekeze mjumbe mmoja kuwa shahidi yao. Isipokuwa kwamba kama kundi linalohusika linawagombea wachache tu wasiozidi kumi, kila mgombea anaweza kumteua mwakilishi wake.

## 6. KUTANGAZA MATOKEO

**a.** Kazi ya kuhesabu kura itafanyika tu wakati ambapo kuna mwanga wa kutosha na wa kuaminika na mahali ambapo kuna ulinzi na usalama madhubuti.

**b.** Kiwango cha kura katika kufikia uamuzi wa mshindi katika uchaguzi usio wa kundi ni zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa. Kura halali zilizopigwa ni kuondoa kura zilizoharibika.

**c.** Katika uchaguzi wa kujaza nafasi nyingi kwa pamoja (uchaguzi wa wajumbe wa Halmashauri) ushindi utahesabiwa kwa kufuata wingi wa kura alizopata muombaji.

**d.** Katika kutangaza matokeo ya kura, mtiririko utakuwa kama ifuatavyo:-

i. Idadi ya kura zilizopigwa
ii. Idadi ya kura zilizoharibika
iii. Idadi ya kura halali zilizopigwa
iv. Matokeo ya kura yatangazwe kuanzia chini yaani aliyepata kura chache zaidi na kuendelea hadi anayeongoza kwa wingi wa kura.
v. Mwisho ni kutangaza rasmi washindi.

**e.** Mwenye mamlaka ya kutangaza matokeo ya uchaguzi ni msimamaizi mkuu wa uchaguzi katika ngazi husika.

Baaada ya kutangazwa kwa matokeo washindi wote watapaswa kupewa hati au cheti cha ushindi.

## 7. NAFASI ZA UONGOZI WA KUTEULIWA

Nafasi za Uongozi zifuatazo zitakuwa za kuteuliwa na mamlaka husika kama ifuatavyo:

**a. Nafasi za kuteuliwa na Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania**

i. Wajumbe Kumi na Tano (15) wa Baraza la Ulamaa
ii. Katibu wa Baraza la Ulamaa
iii. Naibu Katibu wa Baraza la Ulamaa (ambaye pia ndiye atakuwa Katibu wa Mufti)
iv. Qadhi Mkuu
v. Manaibu Wawili (2) wa Qaadhi Mkuu
vi. Katibu wa Qadhi Mkuu
vii. Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu
viii. Katibu Mkuu
ix. Wajumbe Kumi (10) wa Halmashauri Kuu ya Taifa
x. Washauri wa Mufti katika Nyanja mbalimbali
xi. Mshauri wa Uchumi na Mipango wa Baraza Kuu la Waislam wa Tanzania
xii. Manaibu Katibu Wakuu Wawili (Naibu Katibu Mkuu Utawala na Naibu Katibu Mkuu Dini)
xiii. Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Jumuiya za BAKWATA
xiv. Maqadhi wa Mikoa na Wilaya
xv. Makatibu wa Maqadhi wa Mikoa na Wilaya
xvi. Kaimu Mufti miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Ulamaa, inapotokea dharura, atakapokuwa nje ya nchi au atakapokuwa mgonjwa.
xvii. Kukaimisha nafasi yoyote au ngazi yoyote pindi itakapokuwa wazi.

**b. Nafasi za uteuzi utakaofanywa na Baraza la Ulamaa**

i. Masheikh Wa Mikoa
ii. Masheikh wa Wilaya
iii. Kuteua Makatibu wa Mabaraza ya Masheikh wa Mikoa na Wilaya.

**c. Nafasi za uteuzi utakaofanywa na Katibu Mkuu**

i. Makatibu wa Mikoa
ii. Makatibu wa Wilaya
iii. Makatibu wa Mikoa na Wilaya wa Jumuiya za BAKWATA

**d. Nafasi za uteuzi utakaofanywa na Sheikh wa Mkoa**

i. Wajumbe Watatu (3) watakaingia katika Halmashauri ya Mkoa
ii. Kupendekeza wenyeviti wa Jumuiya za BAKWATA ngazi ya Mkoa

**e. Nafasi za uteuzi utakaofanywa na Sheikh wa Wilaya**

i. Wajumbe Watatu (3) watakaoingia katika Halmashauri ya Wilaya
ii. Kupendekeza wenyeviti wa Jumuiya za BAKWATA ngazi ya Wilaya

**f. Nafasi za uteuzi utakaofanywa na Sheikh wa Kata**

i. Wajumbe Watatu (3) watakaoingia katika Halmashauri ya Kata

## 8. MALALAMIKO YA UCHAGUZI

**a.** Kutakuwa na nyaraka mbili za kuwasilisha na kushughulikia malalamiko ya chaguzi zote za BAKWATA ambayo ni Kabla na wakati wa vikao vyenyewe vya uchaguzi na Baada ya uchaguzi kumalizika

**b. Malalamiko kabla na wakati wa mikutano ya uchaguzi**

Malalamiko haya yanaweza kuwasilishwa kabla, au wakati wa vikao vyenyewe vya Uchaguzi, kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:-

i. Mlalamikaji atawasilisha malalamiko yake kwa Katibu wa BAKWATA wa ngazi ile ambapo uchaguzi unafanyika.

ii. Ili kuepuka majungu, na kwa ajili ya kulinda haki, malalamiko yatawasilishwa kwa maandishi, ambayo pia itabidi yaainishe kwa ukamilifu mambo yanayolalamikiwa.

**c. Malalamiko baada ya uchaguzi**

Baada ya kupokea malalamiko, katibu wa BAKWATA wa ngazi inayohusika ataitisha mara moja kikao cha Baraza la Masheikh la ngazi hiyo ambacho ndicho mdhibiti kwa mujibu wa Kanuni hizi.

**d.** Baraza la Masheikh au Baraza la Ulamaa litakuwa na mamlaka ya kushughulikia taarifa za ukiukwaji wa Qur'an na Sunna, maadili au Katiba au Kanuni za BAKWATA wakati wowote, kabla na pia wakati wa uchaguzi wenyewe. Mabaraza haya licha ya majukumu yao ya kisharia yanapaswa pia kudhibiti makosa ya uchaguzi pale yanapofanyika, bila ya kusubiri malalamiko kutolewe baada ya uchaguzi kumalizika.

**e.** Endapo Baraza la Masheikh litabaini kuwepo kwa vitendo vilivyokatazwa katika Kanuni hizi, na ili ratiba ya uchaguzi huo isiathirike, watafanya kikao mara moja ili kutafakari tukio linalohusika na kulitolea uamuzi.

**f.** Malalamiko yoyote ambayo Baraza la Masheikh au Baraza la Ulamaa litaridhika kuwa hayana ukweli yatakataliwa. Lakini kwa malalamiko ambayo yatathibitika kuwa yana ukweli,

Baraza la Masheikh au Ulamaa litakuwa na mamlaka ya kuchukua hatua kwa wahusika kama ifuatavyo:-

i. Pale ambapo kamati husika itaridhika kwamba tuhuma za rushwa dhidi ya mgombea fulani au wakala wake zimethibitika kuwa ni kweli, basi kamati hiyo itapeleka haraka taarifa ya tukio hilo kwa vikao vya Baraza la Masheikh au Baraza la Ulamaa ili hatua zichukuliwe dhidi yao kwa mujibu wa Kanuni.

ii. Kwa wale watuhumiwa wa vitendo ambavyo havihusiani na rushwa lakini bado vinakiuka kanuni za uchaguzi wa BAKWATA, hususani zile zinazokataza matumizi ya mabango, vipeperushi, vurugu za wapambe au matusi na upotoshaji wa makusudi wa sifa za wagombea wengine wanaoshindana nao, hawa watadhibitiwa na kamati husika zilizoteuliwa kwa kuwakemea na kuwaonya mapema waache mara moja kufanya vitendo hivyo, na watuhumiwa hao watalazimika kutii amri hiyo iliyotolewa.

iii. Kwa upande wa watuhumiwa ambao ni viongozi wa BAKWATA wa ngazi yoyote ile waliothibitika kujihusisha na vitendo vya kumbeba na kupendelea miongoni mwa wagombea walioteuliwa rasmi na BAKWATA, kamati ya udhibiti wa ngazi inayohusika itakuwa na mamlaka ya kumkemea na kumpa onyo au onyo na karipio, pamoja na kumtaka kiongozi mhusika aache vitendo vyake hivyo mara moja, na kiongozi aliyetakiwa kufanya hivyo atapaswa kutii amri hiyo.

iv. Endapo makosa ya aina hiyo yatafanywa na kiongozi ambaye ni Katibu wa BAKWATA wa ngazi yoyote, ambae kwa wadhifa wake huu anakuwa pia Msimamizi wa

uchaguzi katika eneo lake au ni afisa, au mtumishi mwingine wa BAKWATA wa ngazi yoyote, kamati ya udhibiti ya juu yake ikisha kuridhika kuwa tuhuma zimethibitika kuwa ni za kweli, itapeleka taarifa ya maandishi mara moja kwa katibu wa ngazi ya juu yake, ambae kutokana na taarifa hiyo atamchukulia hatua za kinidhamu zinazohitajika.

v. Malalamiko yanaweza pia kuwasilishwa baada ya uchaguzi kumalizika kwa kuzingatia utaratibu ulioelezwa katika Kanuni hii.

vi. Mara baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa, Muislamu yeyote aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uongozi inayohusika, endapo anayo malalamiko kuhusu uchaguzi huo, atawasilisha malalamiko yake hayo kwa katibu wa BAKWATA wa ngazi ya juu inayofuata. Isipokuwa kwamba kama uchaguzi unaolalamikiwa ni wa ngazi ya mkoa, malalamiko yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu.

vii. Ili kuepuka majungu, na kwa ajili ya kulinda haki, malalamiko yatawasilishwa kwa maandishi ambayo pia itabidi mlalamikaji ainishe kwa ukamilifu mambo yanayolalamikiwa. Mlalamikaji pia ni lazima ataje majina yake kamili na anuani yake.

**g.** Malalamiko hayo lazima yawasilishwe katika kipindi kisichozidi siku saba (7) tangu siku ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi unaolalamikiwa.

**h.** Kikao kinachoshughulikia malalamiko baada ya uchaguzi kumalizika kwa mujibu wa fasili (i) ya kanuni hizi, kitakuwa vile vile na uwezo wa kusikiliza rufaa kutoka katika kamati

inayohusika, pale ambapo kamati husika ilitoa amri hizo lakini wahusika hawakutii amri hizo, au rufaa kutoka kwa wagombea au kiongozi anayehisi kuwa aliathirika kutokana na maamuzi fulani ya kamati iliyomdhibiti.

**i.** Kila mgombea wa nafasi yoyote ya uongozi azingatie kuwa uchaguzi wa viongozi wa ngazi zote ni suala la kutimiza wajibu ndani ya BAKWATA. Hivyo BAKWATA ina uwezo kamili wa kuyatafutia ufumbuzi malalamiko yote ya uchaguzi yatakayopokelewa bila kuyapeleka mahakamani.

**j.** Malalamiko yatakayowasilishwa kinyume cha kanuni hizi za uchaguzi hayatashughulikiwa.

**k.** Malalamiko ya uchaguzi yatashughulikiwa bila ya kuchelewa na Kamati ya ngazi inayohusika na kutoa uamuzi juu ya malalamiko hayo. Endapo uamuzi uliotolewa unahitaji hatua zichukuliwe ambazo kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA ziko nje ya uwezo wa ngazi inayohusika, Kamati hiyo itatoa taarifa na mapendekezo yake mara moja kwa kikao cha BAKWATA chenye uwezo wa kuchukua hatua iliyopendekezwa.

**l.** Malalamiko yote yanayohusu mambo ya uchaguzi lazima yawe yameshughulikiwa na kumalizwa na vikao vyote vinavyohusika katika muda usiozidi miezi mitatu tangu kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi unaolalamikiwa.

**m.** Baraza la Ulamaa ndicho kikao cha BAKWATA chenye uamuzi wa mwisho katika malalamiko yote yanayohusu uchaguzi wa viongozi wa BAKWATA wa ngazi zote kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## 9. MIIKO KATIKA SHUGHULI ZA UTEUZI NA UCHAGUZI

Maadili na nidhamu ya BAKWATA katika kusimamia na kutekeleza shughuli za uchaguzi lazima kuzingatiwa na wale wote wanaohusika. Hivyo inapaswa kuelewa na kutambua kuwa:-

**a)** Ni kinyume na Uislamu kwa kiongozi, mgombea au Muislamu yeyote kutoa au kupokea rushwa. Kwa ajili hiyo, kiongozi, mgombea yeyote wakati wa uchaguzi akithibitika kuwa ametumia rushwa katika jitihada zake za kuwania nafasi anayoiomba hatateuliwa kugombea nafasi hiyo. Hali kadhalika, mgombea yeyote atakayethibitika kuwa ameshinda uchaguzi kwa njia ya kutoa rushwa, atanyang'anywa ushindi alioupata, na pia atazuiwa kugombea tena katika uchaguzi mwingine wowote kwa muda utakaoamuliwa na Baraza la Ulamaa au atapewa adhabu kubwa zaidi ya hiyo kama itakavyonekana inafaa.

**b)** Ni mwiko kwa kiongozi yeyote wa BAKWATA kuweka mbele maslahi yake binafsi badala ya maslahi ya BAKWATA na Uislamu.

**c)** Hairuhusiwi kwa kiongozi au Muislamu yeyote kuunda vikundi visivyo rasmi ndani ya BAKWATA katika mchakato wa uchaguzi na taratibu rasmi zilizowekwa.

**d)** Hairuhusiwi kwa wapiga kura kupokea misaada ya usafiri, posho n.k kutoka kwa Mgombea yeyote kwa ajili ya kuhudhuria mikutano ya uchaguzi.

**e)** Ni marufuku kwa Jumuiya yoyote inayoongozwa na BAKWATA kujigeuza kuwa kundi la kumjenga au kumbomoa mgombea fulani.

f) Katika ngazi zote za Msikiti hadi Mkoa, pale ambapo kuna nafasi ya wazi ya Uongozi, kama nafasi ya Mwenyikiti wa Halamshauri au mjumbe wa ngazi inayohusika; watateuliwa wagombea wasiozidi watatu ambao watapelekwa kwenye kikao cha uchaguzi kinachohusika.

g) Pale ambapo kuna nafasi nyingi za uongozi wa aina moja, kama wajumbe wa Halmashauri ya Kata, Wilaya au Mkoa watateuliwa wagombea zaidi ya mmoja kwa nafasi zinazotakiwa kujazwa.

h) Haifai kwa kiongozi yeyote au muombaji yeyote wa nafasi ya uongozi au Muislamu aliyekabidhiwa dhamana ya usimamizi au uangalizi wa uteuzi/uchaguzi, kufanya vitendo vya ukiukaji wa Kanuni na taratibu za uchaguzi.

i) Ni marufuku kufanya vitendo au kutumia vishawishi vya aina yoyote ile kwa malengo ya kupata kura.

j) Ni marufuku mgombea kufanya hujuma yoyote ile dhidi ya mgombea mwingine.

k) BAKWATA haitaruhusu na inalaani vitendo vyenye nia ya kupakana matope.

l) Kumbukumbu za uchujaji na uteuzi wa wagombea ni siri ya BAKWATA.

m) Ni marufuku kwa viongozi na watendaji wa BAKWATA wa ngazi zote kuwatembeza baadhi ya wagombea ndani ya maeneo yao kwa nia ya kuwatambulisha wapiga kura. Kiongozi au mtendaji atakaebainika amekiuka katazo hili atachukuliwa hatua kali za kinidhamu; pia mgombea huyo ataondolewa katika orodha ya wagombea.

**n)** Kiongozi au Muislam yeyote atakaethibitika kuwa amevunja kifungu chochote cha miiko hii ataadhibiwa ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa ushindi alioupata na kukatazwa kugombea uongozi kwa muda utakaowekwa.

## SURA YA PILI

## UCHAGUZI WA VIONGOZI WA NGAZI YA MSIKITI

### 10. MSIKITI

**a.** Kwa madhumuni ya kanuni hizi na katiba ya BAKWATA, "Msikiti" ni ngazi ya awali kabisa na inajumuisha Waislamu wote sajiliwa wanaoishi katika eneo hilo na kuswali katika msikiti huo.

**b.** Misikiti inamaanisha na kujumuisha misikiti yote iliopo Tanzania bara yenye kumilikiwa, kuendeshwa na kusimamiwa kufuatana na miongozo, taratibu, Kanuni na Katiba ya BAKWATA.

### 11. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI ZA UONGOZI NGAZI YA MSIKITI

**a.** Kila Muislamu anaeishi na kuswali katika msikiti huo na mwenye sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya BAKWATA na ambae anajua kusoma na kuandika anayo haki kuomba nafasi zifuatazo: -

i. Imam
ii. Naibu Imam
iii. Katibu
iv. Mhazini
v. Wajumbe wa Kamati ya Msikiti
vi. Wajumbe wa Usuluhishi wa Migogoro.
vii. Wajumbe Wawili wa kuwakilisha kwenye kata

**b.** Muombaji wa nafasi ya uongozi wa ngazi ya msikiti atajaza fomu maalum iliyoandaliwa kwa ajili ya uchaguzi na kuiwasilisha kwa Katibu wa kata ambapo msikiti huo upo katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi unaohusika.

**c.** Kamati ya Msikiti itajadili na kutoa mapendekezo kwa Baraza la Masheikh la Kata kuhusu Waislamu wanaoomba nafasi za uongozi katika Msikiti huo. Aidha Halmashauri ya kata itafikiria na kutoa mapendekezo kwa Baraza la Masheikh la kata juu ya Waislamu wanaoomba nafasi za uongozi wa BAKWATA katika Msikiti huo.

**d.** Baraza la Masheikh la kata litapokea, kujadili na kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea walioomba kugombea katika uchaguzi wa ngazi ya msikiti.

**e.** Majina yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho yatarudishwa kwenye msikiti unaohusika ili uchaguzi ufanyike kwa kuzingatia ratiba iliyopangwa ya uchaguzi.

## 12. UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA MSIKITI

**a.** Majina yaliyopitishwa na Baraza la Masheikh la Kata ambayo ndio uteuzi wa mwisho yatapigiwa kura katika uchaguzi kwenye msikiti husika ili kupata viongozi.

**b.** Endapo wagombea waliopitishwa ni zaidi ya mmoja wajumbe watapiga kura za siri kumchagua kiongozi wa msikiti wanaemtaka kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa kwa madhumuni hayo.

**c.** Endapo idadi ya kura italingana, watapigiwa kura tena mpaka apatikane mwenye kura nyingi zaidi na huyo ndie atakaekuwa mshindi.

## SURA YA TATU
## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA KATA

### 13. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI YA UONGOZI WA KATA

**a.** Kila Muislamu mwenye kuishi katika kata ambae anatimiza masharti yote kwa mujibu wa Katiba ya BAKWATA na anaejua kusoma na kuandika anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi katika kata.

i. Mwenyekiti wa kata
ii. Katibu wa Kata
iii. Wajumbe Saba (7) wa Baraza la Masheikh la Kata
iv. Wajumbe Kumi (10) wa Halmashauri ya Kata
v. Wajumbe Wawili (2) wa Halmashauri ya Wilaya

**b.** Wagombea wote watajaza fomu zinazohusika na kuziwasilisha kwa Katibu wa Kata katika kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi wa ngazi ya kata. Nakala moja ya fomu ya kila muombaji itabaki kwenye kikao cha awali na ya pili kwenye kikao cha uteuzi wa mwisho.

**c.** Baraza la Masheikh la Kata litajadili na kuchunguza sifa za waombaji wa nafasi zote za uongozi wa kata na kupeleka maoni yao juu ya waombaji wote katika Baraza la Masheikh la Wilaya. Maoni haya yatakuwa yameandikwa kwenye fomu ya muombaji.

**d.** Majina yaliyopitishwa katika uamuzi wa mwisho yatarudishwa kwenye kata inayohusika ili uchaguzi ufanyike. Katibu wa kata lazima awe na idadi sahihi kabisa ya wajumbe wanaopaswa kuhudhuria katika Mkutano wa uchaguzi kwa mujibu wa Katiba.

## 14. UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA KATA

**a.** Baada ya majina ya wagombea yaliyochujwa kuwasilishwa kwenye Kata kutaitishwa Mkutano Mkuu wa Kata kwaajili ya Uchaguzi.

**b.** Msimamizi wa uchaguzi wa Kata ni lazima awe na idadi sahihi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata wanaopaswa kuhudhuria Mkutano huo. Uchaguzi utasimamiwa na katibu wa Wilaya na utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao: -

i. Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa kata yawe yamepangwa kwa kufuata alfabeti.

ii. Katibu wa BAKWATA wa Wilaya atathibitisha orodha ya wajumbe waliohudhuria na kutangaza kutimia kwa akidi ya wajumbe wa mkutano huo.

iii. Mara baada ya akidi ya wajumbe kuthibitishwa, mkutano utamchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao kuwa mwenyekiti wa muda wa mkutano huo. Atakechaguliwa asiwe mmoja ya wagombea wa nafasi yoyote ya uongozi. Uchaguzi huo unaweza kufanyika kwa njia ya kunyoosha mikono juu na kuihesabu.

iv. Wagombea wote watajieleza kuanzia nafasi ya katibu, kila mgombea atapewa nafasi ya kutoa maelezo kwenye mkutano huo na wajumbe watapewa nafasi ya kuuliza maswali yasiozidi matatu, kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile muombaji hatahudhuria katika mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

v. Baada ya wagombea wote kutoa maelezo yao, mkutano utawachagua viongozi kama ilivyoelezwa katika kanuni hizi. Endapo mgombea mmoja tu ndie aliyepitishwa katika uteuzi wa mwisho, mkutano utampigia kura za siri za "ndiyo" au "Hapana" kwa kutumia karatasi maalum za kura zilizoandaliwa kwa ajili hiyo. Matokeo yatahifadhiwa.

vi. Mkutano utaendelea kwa utaratibu huo huo kwa uchaguzi wa wajumbe wa Halmashuri ya kata, nafasi kumi na Mbili (12). Wajumbe Kumi (10) wa Halmashauri ya kata na Wajumbe Wawili (2) wawakilishi katika Mkutano Mkuu wa Wilaya.

vii. Kisha yatasomwa mapendekezo ya wajumbe watatu (3) wa Halmashauri waliyopendekezwa na Sheikh wa Kata.

viii. Uchaguzi wa wajumbe wa nafasi zote utakapomalizika na kura kuhesabiwa, ndipo matokeo yote kwa pamoja yatatangazwa. Matokeo ya Katibu wa Kata yatakuwa ya mwisho kutangazwa. Wajumbe wawili (2) wawakilishi wa mkutano mkuu wa wilaya watatangazwa kwanza.

## SURA YA NNE
## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA WILAYA

### 15. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI ZA UONGOZI NGAZI YA WILAYA

**a.** Muislamu yeyote ambae anafuata Qur'an na mwenendo wa Mtume Muhammad (swala llahu alaihi wasalaam) na kutimiza sifa za uongozi kwa mujibu wa katiba ya BAKWATA toleo la mwaka 1999, ibara ya 80 na ambae anajua kusoma na kuandika basi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi wa wilaya:-

i. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya
ii. Masheikh saba (7) watakaoingia katika Baraza la Masheikh la Wilaya
iii. Wajumbe kumi (10) wa Halmashauri ya wilaya

**b.** Muombaji wa nafasi ya uongozi wa ngazi ya Wilaya atajaza fomu maalum inayohusika kwa nafasi anayoiomba, na kuwasilisha fomu yake kwa katibu wa BAKWATA wa Wilaya, kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi wa ngazi ya wilaya. Nakala moja ya fomu itabaki kwenye kikao cha awali kinachowajadili waombaji na ya pili itahifadhiwa na kikao cha uteuzi wa mwisho.

**c.** Baraza la Masheikh la Wilaya litachunguza sifa za waombaji wa nafasi zote za uongozi wa ngazi ya wilaya. Katika kuitekeleza kazi hiyo, kamati ya uchaguzi itahakikisha kwamba fomu zote zimejazwa kwa usahihi.

**d.** Baada ya ujazaji wa fomu kukamilika, Baraza la Masheikh la Wilaya, litatoa mapendekezo yake juu ya kila muombaji kwenye sehemu inayohusika. Mapendekezo ya hayo

yatafikishwa kwenye kikao cha Baraza la masheikh la Mkoa.

**16. UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA WILAYA**

**a.** Majina yote yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho na vikao vinavyohusika yatarejeshwa kwa Msimamizi wa uchaguzi wa Wilaya inayohusika ili uchaguzi ufanyike. Msimamizi wa uchaguzi wa Wilaya ni lazima awe na idadi sahihi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya unaopaswa kuhudhuria Mkutano huo.

**b.** Mkutano mkuu wa wilaya utakaofanyika kwa madhumuni ya uchaguzi utasimamiwa na Msimamizi wa uchaguzi ambaye ni Katibu wa Mkoa na utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

i. Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa wilaya yawe yamepangwa kufuata alfabeti.

ii. Msimamizi wa uchaguzi atathibitisha orodha ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa uchaguzi na kisha atatangaza kwamba akidi ya wajumbe wa mkutano imetimia.

iii. Baada ya tangazo la akidi ya wajumbe kutimia, itakuwa ni Kumchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwa wajumbe wa mkutano mkuu wa ucahguzi kuwa Mwenyekiti wa muda, na uchaguzi huo unaweza kufanyika kwa njia ya kuinua mikono na kuihesabu.

iv. Endapo mgombea yeyote atashindwa kuhudhuria mkutano huo kwa sababu yoyote basi maelezo yake

yatasomwa na atakuwa na haki ya kupigiwa kura lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

v. Mkutano utaendelea kwa utaratibu huo huo kwa uchaguzi wa nafasi mbalimbali katika ngazi ya Wilaya kwa kuzingatia utaratibu kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Wajumbe Kumi (10) wa halmashauri ya Wilaya na Wajumbe Saba (7) watakaoingia katika Baraza la Masheikh la Wilaya.

vi. Uchaguzi wa wajumbe wa nafasi zote ukimalizika na kura zote kuhesabiwa ndipo matokeo ya nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya yatatangazwa mwisho.

## SURA YA TANO
## UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI YA MKOA

### 17. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI ZA UONGOZI NGAZI YA MKOA

**a.** Muislamu yeyote ambae anafuata Qur'an na mwenendo wa Mtume Muhammad (swala llahu alaihi wasalaam) na kutimiza sifa za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya BAKWATA ya mwaka 1999, toleo la 2018, ibara ya 80 na ambae anajua kusoma na kuandika basi anayo haki ya kuomba nafasi zifuatazo za uongozi wa Mkoa:-

i. Mwenyekiti wa Mkoa (1)
ii. Mjumbe (1) wa Halmashauri Kuu anaewakilisha Mkoa
iii. Masheikh Tisa (9) watakaoingia katika Baraza la Masheikh la Mkoa
iv. Wajumbe kumi (10) wa Halmashauri ya Mkoa

**b.** Muombaji wa nafasi ya uongozi wa ngazi ya mkoa atajaza fomu maalum inayohusika kwa nafasi anayoiomba, na kuwasilisha fomu yake kwa katibu wa BAKWATA wa Mkoa, kwa mujibu wa ratiba ya uchaguziwa ngazi ya Mkoa. Nakala moja ya fomu itabaki kwenye kikao cha awali kinachowajadili waombaji na pili itahifadhiwa na kikao cha uteuzi wa mwisho.

**c.** Baraza la Masheikh la Mkoa litachunguza sifa za waombaji wa nafasi zote za uongozi wa ngazi ya Mkoa. Katika kuitekeleza kazi hiyo, Baraza la Masheikh litahakikisha kwamba fomu zote zimejazwa kwa usahihi.

**d.** Baada ya ujazaji wa fomu kukamilika, Baraza la Masheikh la Mkoa, litatoa mapendekezo yake juu ya kila muombaji

kwenye sehemu inayohusika. Mapendekezo hayo yatafikishwa kwenye kikao cha Baraza la Ulamaa.

**18. UTARATIBU WA UCHAGUZI NGAZI YA MKOA**

**a.** Majina yote yaliyopitishwa katika uteuzi wa mwisho wa vikao vinavyohusika yatafikishwa kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa ili uchaguzi ufanyike.

**b.** Mkutano mkuu wa mkoa utakaofanyika kwa madhumuni ya uchaguzi, utasimamiwa na Afisa atakaeteuliwa na Katibu Mkuu ambae ndie Msimamizi Mkuu wa uchaguzi na utaendeshwa kwa utaratibu ufuatao:-

i. Majina ya wagombea kwa kila nafasi ya uongozi wa Mkoa yawe yamepangwa kufuata alfabeti.

ii. Msimamizi wa uchaguzi atathibitisha orodha ya wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi na kutangaza kutimia kwa akidi ya wajumbe wa Mkutano huo.

iii. Baada ya tangazo la akidi ya mkutano kutimia, itakuwa ni Kumchagua mjumbe mmoja kutoka miongoni mwao wajumbe wa mkutano huo kuwa Mwenyekiti wa muda.

iv. Baada ya hapo mkutano utaanza kumsikiliza mgombea mmoja mmoja kujieleza. Kila mgombea atapewa nafasi ya kuulizwa maswali yasiyozidi matatu, kama yapo. Endapo kwa sababu yoyote ile muombaji hatahudhuria katika mkutano huo, maelezo yake yatasomwa lakini mkutano mwingine hautaitishwa tena ili kumsikiliza.

v. Wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mkoa watajieleza kwanza na mara baada ya maelezo yao wote, kura zitapigwa. Kisha Mkutano utaendelea na utaratibu huo huo kwa nafasi ya wajumbe wa Baraza la

Masheikh wa Mkoa, Halmashauri ya Mkoa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa.

vi. Matokeo ya kura yatatangazwa yote kwa pamoja baada ya kura za kila muombaji katika nafasi zote kuhesabiwa. Matangazo ya matokeo yataanza na nafasi ya wajumbe wa Halmashauri ya Mkoa, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, wajumbe wa Baraza la Masheikh la Mkoa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mkoa.

## SURA YA SITA

## MKUTANO MKUU WA TAIFA NA MENGINEYO

### 19. MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA TAIFA

**a.** Kupokea na kuthibitisha uchaguzi wa Mufti kama ulivyoamuliwa na Tume ya Dini.

**b.** Kuwathibitisha Wajumbe wa Baraza la Wadhamini kama walivyoteuliwa na Baraza la Ulamaa

**c.** Utawathibitisha wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kama walivyochaguliwa na Mikoa husika.

### 20. UCHAGUZI WA KUJAZA NAFASI ZILIZOACHWA WAZI

**a.** Nafasi ya uongozi itakuwa wazi endapo litatokea mojawapo katika matukio yafuatayo kumhusu kiongozi aliyekuwa ameshika nafasi hiyo:-

i. Atajiuzulu mwenyewe
ii. Atafariki dunia
iii. Atapoteza sifa za uongozi

**b.** Mara baada ya nafasi ya kiongozi kuwa wazi, katibu wa BAKWATA wa ngazi husika atafanya mambo yafuatayo kwa idhini ya Katibu wa kikao kilichofanya uteuzi wa mwisho wa wagombea wa nafasi hiyo iliyoachwa wazi: -

i. Atatangaza nafasi hiyo ili Waislamu wanaopenda na wenye sifa bora za uongozi kama ilivyoelezwa katika kanuni hizi waweze kujaza fomu za kuomba nafasi hiyo.
ii. Ataweka ratiba ya uchaguzi wa kujaza nafasi hiyo.

**c.** Ratiba ya uchaguzi ya kujaza nafasi za uongozi zilizowachwa wazi itapaswa kuzingatia yafuatayo: -

i. Kwanza nafasi yoyote ya uongozi inapoachwa wazi inatakiwa ijazwe kwa kufuata utaratibu uliowekwa.

ii. Kwa maelekezo ya kanuni za uchaguzi wa BAKWATA na maelezo ya katiba juu ya ujazaji wa nafasi za uongozi zinapoachwa wazi katika ngazi mbalimbali za uongozi yanatekelezwa ipasavyo.

iii. Katibu wa BAKWATA anayeandaa uchaguzi wa kujaza nafasi iliyo wazi, awasilishe haraka ratiba ya uchaguzi kwa Katibu wa kikao kinachofanya uteuzi wa mwisho wa wagombea ili tangazo la kujaza nafasi hiyo iwekwe ndani ya ratiba ya uchaguzi utakaotolewa idhini ya kutangazwa.